

# Familia na wapendwao katika usalama na ulinzi wa Watetezi wa haki za binadamu walio katika hali ya hatari

Familia na wapendwa ni muhimu kwa maisha ya watetezi wa haki za binadamu. Kutoka kwa majadiliano na watetezi wa haki za binadamu wa Kolombia, Meksiko, Misri, Kenya na Indonesia, sera hii fupi inazungumzia njia ngumu ambazo familia na wapendwa wanahusika katika usalama na ulinzi wa watetezi walio katika hali ya hatari.

## Familia na wapendwao waliolengwa kwa vitisho na mashambulizi

Katika nchi zote tano, familia za watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakilengwa na wahalifu ili kudakiza maisha ya watetezi na kuacha kazi zao. Watetezi wanazingatia usalama wa familia na wapendwa wanapofikiri juu ya usalama wao wenyewe. Wanasema kuwa jamii zao wamepataata vitisho vya kifo na kunyayaswa kwa simu; wamefuatwa na kudhalilishwa hadharani. Katika baadhi nyingine, wamejeruhiwa na hata kuuawa. Mtetezi mwanamke anayefanya kazi ya haki za wale waliopotea na waathiriwa wa ukatili nchini Kolombia alisema: "Pia kuna vidokezo yenye majina ya wajukuu wangu na risasi zilizogandishwa: walisema, 'kutakuwa na zingine kamaingine kama hizi kamakama hautawacha hiyo kazi na ukimye."

Vitisho na mashambulizi juu ya familia ni chanzo cha kutokuwa na uhakika mkubwa, wasiwasi na shida. Mwanamke mlinzi anayefanya kazi ya kulinda haki za wanawake, walioteweka kwa nguvu na unyanyasaji dhidi ya wanawake huko Meksiko, alisema:

> *Kutokuwa na uhakika; unatoka nyumbani, unawaaga familia yako kwaheri na hujui kama utarudi kama utarudi ... si kama hatari ya kupoteza kazi yako, gari, bidhaa; kazi yetu inatuweka katika cheneocheneo chacha kupoteza maisha yetu au maisha ya jamii.*

Usalama ambao watetezi wanaishi nao mara nyingi huathirika, na sio tu njia wanayofanya kazi yao bali pia vile wanavyoishi maisha yao, tabia zao za kila siku, mienendo ya familia, na mahusiano yao na watu wengine.

> *Ilibidi tubadilishe maisha yetu, uhusiano na familia yetu uliathiriwa, uhusiano na mpenzi wangu ... yeye na familia yangu waliathiriwa Zaidi kuliko mimi ... kwa sababu [serikali] ilikuwa na habari kuhusu shule zote mpwa wangu alikuwa amesomea ... namba za simu za mkononi ambazo baba yangu alikuwa ametumia miaka 7 iliyopita ... nililazimishwa kuzungumza na familia yangu ... mikakati [ya usalama] ilipitishwa na familia yangu ... hatukujuaa kama shambulio litakuja dhidi ya yule aliyeonekana zaidi [mimi] au dhidi ya mwingine katika familia yangu.*
>
> **Mtetezi wa kiume anayefanya kazi za haki zya elimu, ardhi, haki za asili, watu waliopotea na mauaji yasiyo ya halali huko Meksiko**

Watetezi pia wanahisi hatia kali kwamba familia zao lazima wachukue hatari ambazo zinazotoka kwa kazi zao. Ili kuwalinda, watetezi wengine hufanya uamuzi kukata au kuzuia kuwasiliana na wapendwa wao, au kuwatuma mbali ili kupunguza vitisho.

## Familia na wapendwao kama sababu ya kutetea haki za binadamu

Watetezi wengi huendeleza na kutetea haki za kibinadamu kwa ajili ya familia zao na wapendwao. Katika hali nyingine, wanatafuta haki kwa wapendwa ambao wameuawa au kutoweka. Akielezea ukubwa wa familia katika kazi yake ya haki za binadamu, mlinzi kutoka Colombia anayefanya kazi kwa haki za ardhi na haki za waathirika wa unyanyasaji alisema:

> *Nilianza [kazi hii] kwa sababu niliona umuhimu wa jamii na familia yangu. Na katika hayo yote, tuli telekezwa na Serikali. Hakukuwa na msaada wa Serikali pahali ambapo niliishi. Maofisa wa umma waliikuwa wanatutusi, na kulikuwa na makundi mbalimbali waliyokuwa wakitumia silaha ... Baba yangu alikuwa na biashara ambayo ilishambuliwa na wakundi ya wahuni na wanajeshi mpaka alilazimishwa kuifunga ... Ndugu yangu aliuawa kwa kuwa mwanaharakati wa kijamii . Baba yangu aliuawa pia. Kwa hiyo, niliamua kufanya kazi ya kutetea haki za binadamu.*

Watetezi wanaona jinsi vurugu inavyoharibu familia na wanawajibika kwa kuzungumza na kuipinga. Wanageuza hasara, huzuni na hasira yao kuwa nguvu na motisha kwa kazi yao. Mwanamke mlinzi anayetafuta haki ya mtoto wake ambaye aliuawa nchini Kolombia alisema,

> *Tumekuwa wagonjwa wakati mwingine juu ya hii hali, na tumepoteza watu wengine wa familia; mwana wangu wa kiume mwenye umri kubwa alikufa moyo juu ya kile kilichotokea ... Hata hivyo, ndani ya uchovu, tunapokutana na kutafakari juu ya vitu, tunapata nguvu ... Kumbukumbu la watoto wetu linataka tuendelee. [Wahalifu] hufanya mambo haya yote ili tuweze kuacha, lakini upendo wa mama ni wa milele.*

## Familia na wapendwao kama vyanzo vya usaidizi

Kwa watetezi wengi, familia ni muhimu kwa hatua zao za ulinzi na usalama. Wajumbe wa familia hufanya kazi muhimu kwa ajili ya mawasiliano wakati wa hatari, kulipa dhamana ndio watetezi waachiliwe na magereza, kuwapa makao ya muda mfupi, na msaada muhimu wa akili na kihisia. Akizungumzia juu ya kilichomfanya kujisikie salama, mlinzi wa kiume kutoka Indonesia anayefanya kazi ya kulinda uhuru wa kujieleza na haki za ardhi alisema:

> *Ninajiskia ni kiwa salama ikiwa naweza kukaa na familia. Familia yangu inaelewa kila kitu ninachofanya. Ninajenga ufahamu wa hatari katika familia yangu. Pia ninajisikia nilkiwa salama ikiwa nina ulinzi wa kijamii katika jumuiya au kijiji. Ni juu ya kujenga ulinzi ya kusaidiana kati yetu.*

Familia zinajua zaidi kazi ya watetezi na sababu zao za kuifanya, ndivyo wanaweza kujilinda na kuwasaidia.

> *Msaada wa familia yangu ni muhimu. Nadhani ni muhimu kwamba wanajua kile ninachokifanya, na kwamba wanaelewa hatari ile kazi yangu inahusisha. Ni muhimu kwangu kwamba wanaunga mkono kile ninachokifanya. Hata kuna wazazi wengine ambao wako kwenye kikundi chetu; wanasaidia kwa maandamano na shughuli tunayofanya. Hii ni muhimu kwa kikundi.*
>
> **Mwanamke mwanaharakati anayehusika na haki za mazingira nchini Kolombia**

## Familia na wapendwao kama vyanzo vya madhara

Watetezi wengine walizungumzia uchungu wao juu ya familia kukataa kazi zao.


Wakati mwingine, anafamilia wa watetezi wa haki za binadamu wanafikiria na kuweka kwa ndani utegemezi iliyowekwa na serekali kwa vyombo vya habari. Mtetezi wa kike anayefanya kazi kwa haki za wanawake huko Misri, alielezea, "Ikiwa wanakupaka matope, familia yako itakuhimiza uache kufanya kazi. Hapa wanatumia jinsi hii sana kuliko vurugu. Wanatumia familia kama kadi dhidi yangu."

Wakati mwingine, wanajamii hutenga watetezi baada ya shambulizi. juu ya hofu. Mwanamke mlinzi anayefanya kazi ya kufuatilia mauaji yasiyo halali nchini Kenya, ambaye mtoto wake alipigwa sana, kutekwa nyaraa na kuuawa kwa kulipiza kisasi kwa kazi yake alisema, "Badala ya [jumuiya] kunisaidia, walinitenga kwa sababu walihisi kuwa mimi nawahamisishia vitisho."

> *Kutenga kwa jamii ya watetezi wa haki za binadamu sio jambo njema. Kuhukumiwa na watu karibu na wewe na familia yako si hisia nzuri. Mimi binafsi naona kuwa hii ni hatari zaidi - unyanyapaa wa kijamii.*
>
> **Mwanamke mlinzi anayefanya kazi kwa uhuru wa vyombo vya habari na haki za wanawake huko Misri**

Maoni ya jinsia juu ya kile kinachofanya 'mwanamke mzuri' na 'binti nzuri' huathiri jinsi familia zinavyoelezea kazi ya wanawake watetezi. Alipoulizwa kutafakari vile jinsi jamii inavyoona watetezi wa haki za binadamu, mwanamke mlinzi anayefanya kazi ya haki za kiraia na kisiasa huko Misri alisema:

> *Ninajaribu kufikiria mambo yote ambayo mama yangu anasema, kwa sababu kwangu yeye ni kioo cha ukweli cha jamii, ambayo siingilii ... Tunaonekana kama wakosa dini, washerati, wenye hasira na kila mtu na kila kitu kutoka Mungu mpaka jamii na serikali. Tunaonekana kama watumwa wa tamaduni za nchi za magharibi.*



Matarajio ya jinsia pia huweza kusababisha vurugu za mpenzi na unyanyasaji wa kijinsia kwenye kazi. Watetezi wanawake wanajitahidi kupata nafasi za kukabiliana na kuongea juu ya vurugu kutoka familia zao na jumuiya za haki za binadamu. Kama mlinzi wa mwanamke huko Mexico alivyo ona,,

> *Katika kazi yangu na watetezi wa kike wa haki za binadamu, nimegundua kuwa unyanyasaji wa jinsia kwenye mashirika na familia iko hai ... wakati vurugu inatoka kwa familia ya karibu na kwenye mashirika ya kazi ya watetezi inakuwa ngumu sana... hii ni suala la kimuundo; ni kuhusu uzazi wa vurugu za jinsia katika nyanja zote za maisha kwa watetezi wa kike wa haki za binadamu. Hii mambo inawekwa kama ni na kawaida na kunyanyapaa. Kuzungumza waziwazi juu ya hili inamaanisha kuhoji ushirikiano wa kisiasa wa majadiliano na vitendo katika haki za binadamu ndani ya mashirika.*

Watetezi wa LGBTIQ pia wanakabiliwa na shida za kukataliwa na familia na wapendwao juu ya mwelekeo na utambulisho wa kijinsia. Wao wamelazimishwa kutoka nyumba zao, kutishiwa na wanafamilia, kutengwa na ijamii, kusimamishwa kazi, na kufanywa kuishi kwa hofu ya kupatikana na wapendwa wao. Akielezea vile mtetezi mwenye hiari wa LGBTIQ kutoka Misri alivoona:

> *Familia ya mtetezi mwenye hiari ambaye alijiunga na timu yetu alijua kuhusu mwelekeo wake wa kijinsia na alijua kwamba alikuwa akifanya kazi kwa sababu ya LGBTI ... familia yake ilimfungilia kwenye nyumba alafu akampeleka chumba cha wazimu. Mama yake ndiye alitutishia, akisema, ikiwa hatutaenda karibu na binti yake hatatudhuru [kwa kuwaambia polisi kazi ile tunafanya].*

Katika hali nyingine, familia hubadili mawazo yao. Mtetezi wa mwanamke wa trans nchini Kenya alielezea jinsi alivyokataliwa na familia yake lakini hii ilibadilika, akisema, "Walibadilisha mawazo pole pole na tumeona njia za kukutana na kuzungumza." Hii inaonyesha umuhimu wa kufanya kazi na familia kushughulikia mawazo mabaya juu ya kazi za haki za binadamu, jinsia, haki za LGBTIQ * na utambulisho mwingine. Ni vizuri kujenga na kuunga mkono kazi ya watetezi hawa.

## Umuhimu wa familia na wapendwao kwa usalama na ulinzi wa watetezi

Familia za watetezi na wapendwao ni muhimu kwa hisia ya nafsi, utambulisho, usalama, ustawi na kusudi, zina haja ya kuingizwa katika hatua za ulinzi. Kama mtetezi wa kiume juu ya haki za kijamii na kiuchumi na haki za ardhi nchini Kolombia alisema:

> *Wanapokupa nguo ya kuzuia risas au simu ya mkononi, hii ni ya kulinda mtu binafsi, lakini ... Watu wote walio karibu nami pia wanaweza kuwa katika hatari kwa sababu ya kazi yangu ... Kuna haja ya kuwa na ulinzi wa kijumiya pamoja ... Je, itakuwa aje kama ni mimi tu niko na ulini, je  familia yangu Katika Choco, tunaposema kuhusu familia, tunazungumzia familia kubwa. Tunazungumzia kuhusu familia ya mchakato mzima.*

Kwa watetezi wa LGBTIQ, kazi yao inahusisha kujadili fikra za kitamaduni za familia inahusu nani, na pia kulinda utakatifu wa familia hizo.

Watetezi walizungumzia juu ya haja ya kujenga mbinu ya kuunga mkono kwa familia na wapendwao. Hii mbinu huchanganya hatua za usalama wa kimwili, usalama wa kifedha, na tegemeza ya kisaikolojia, wakati wowote kama mtetezi ako ama hayuko, akiwao kizuizini, akiwa amekuhamishwa au hata kuuawa.

Wakili wa haki za binadamu huko Misri alieleza baadhi ya mipango yake ya usalama:

> *Nimezungumza na baba na pia kakangu mkubwa  kuwa nikikamatwa tumekubaliana nani ambaye atakuwa wakili wangu na pia orodha ya wakili wengine ambao wanaweza kunilsaidia ikiwa wakili wa kwanza pia ako gerezani. Wana majina yao na namba za simu, pia nimewauliza familia yangu wasinitembelee gerezani ila kuwasiliana na wakili kupata taarifa yoyote wanayohitaji kuhusu mimi .... Niko na kitengo cha dharura wakati nitakamatwa, pesa kwa ajili ya mke na binti yangu kuwa na uwezo wa kuishi... niko na uhakika kuwa jumuiya ya wakili iko imara sana na inaunga mkono kesi za wanaharakati.*

Usalama, huduma na msaada ya familia na wapendwao ni muhimu katika ulinzi wa watetezi katika hatari. Kama mtetezi kutoka Kenya alivyosema, alipoulizwa nini anafikiria juu ya usalama wake: "Mimi niko na usalama? Je! Familia yangu iko salama? Maisha ya familia yangu inakuja kwanza, kabla yangu."

## Vidokezo kwa watendaji

- Kutambua umuhimu wa familia na wapendwao kwa utambulisho, ustawi, usalama na ulinzi wa watetezi.
- Ni muhimu kufikiria mawazo juu ya 'familia' ni nani, ili kuruhusu watetezi kufafanua ambavyo wanafikiria juu ya familia.
- Weka familia na wapendwao katika mipango ya usalama na hatua za ulinzi kwa watetezi kutoka mwanzo mpaka wakati mipango itatekelezwa.
- Tengeneza mipangon za msaada wa dharura na za muda mrefu kwa wanachama na wapendwao, ikizingatia kutokuwepo kwa watetezi.
- Chambua madhara ya hatua za ulinzi kwa familia na wapendwao, haswa watoto, ili kupunguza madhara mabaya.
- Tambua kuwa familia na jamii zinaweza kuwa vyanzo vya madhara kwa watetezi. Endeleza hatua za kukabiliana na unyanyapaji na kujenga ridhaa kwa kazi na utambulisho wa watetezi kati ya familia zao na wapendwao.
- Tambua umuhimu wa kuunganisha familia ambazo zimeathiriwa na vurugu na maumivu na kujenga miundo ya msaada pamoja.

**Bottom section below needs translating**

### Tentang Proyek ini:

Ringkasan Kebijakan ini didasarkan pada temuan penelitian dari proyek berjudul ‘Menjelajahi Resiko, Mengelola Keamanan, dan Menerima Dukungan’ yang menelaah pengalaman para pembela HAM yang menghadapi resiko di Indonesia. Penelitian ini juga dilakukan di Kolombia, Meksiko, Mesir, dan Kenya.

Wawancara dan survei terhadap lebih dari 400 pembela HAM dilakukan antara bulan Juli 2015 dan November 2016.

UNIVERSITY of York

Centre for Applied Human Rights
University of York
Yorkshire House
6 Innovation Close, York Science Park
Heslington, York YO10 5ZF
United Kingdom

+44 (0)1904 325830
cahr-admin@york.ac.uk
***york.ac.uk/cahr***

**Peneliti Utama**
Alice M. Nah

**Tim Peneliti**
Sherif Azer
Patricia Bartley
Peter Cousins
Indria Fernida
Kholoud Hafez
Budi Hernawan
Irina Ichim
Katrina Maliamauv
Erick Monterrosas
Patrick Mutahi
Paola Pacheco Ruiz
Emily Schmitz

**Untuk informasi selanjutnya:**
***securityofdefendersproject.org***
security-of-defenders-project@york.ac.uk

**Referensi**

Maliamauv, K. and Nah, A.M. (2018) Families and Loved Ones in the Security and Protection of Defenders at Risk, Human Rights Defender Hub Policy Brief 4, Centre for Applied Human Rights, University of York: York, available at ***www.securityofdefendersproject.org***

**Copy-editing**
Dewi English

**Ilustrasi**
Lara Luna Bartley

**Desain**
Design and Print Solutions

41392 – york.ac.uk/design-print-solutions